


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MEI 7, 2019

KUMFIKISHA MAHAKAMANI ALIYEKUWA AFISA BIASHARA WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU BI. GLADNESS ELISAMIA KITOMARY

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inatarajia kumfikisha mahakamani Bi. Gladness Elisamia Kitomary aliyekuwa afisa biashara wa halmashauri ya wilaya ya Meru leo tarehe 07.05.2019 katika mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kwa kosa la kutumia cheti cha kughushi k/f cha 342 cha sheria ya kanuni za adhabu namba 16/1985 Rev.2002.

Ufafanuzi wa kosa:

TAKUKURU Mkoa wa Arusha ilipokea taarifa kutoka kwa raia mwema ikimtuhumu Bi. Gladness Elisamia Kitomary aliyekuwa afisa biashara wa halmashauri ya wilaya ya Meru kwamba alighushi cheti cha kidato cha nne kinachooonesha kuwa alihitimu elimu ya sekondari katika shule ya sekondari Enaboishu mwaka 1992 na kupata daraja la III.

Uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba Bi. Gladness alipata alama sifuri (0) katika elimu hiyo ya sekondari na pia Bi. Gladness alitumia cheti hicho kilichoghushiwa kupata ajira katika halmashauri ya wilaya ya Meru mnamo mwaka 2009.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inatumia fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali ambao wameamua kwa dhati kuunga mkono Jitihada za Serikali katika kuzuia na kupambana na Rushwa katika mkoa wa Arusha.

Kipekee natoa pongezi kwa mkuu wa jeshi la polisi mkoa wa Arusha ambaye hivi karibuni ameahidi kuwashughulikia au kuwachukulia hatua askari wa usalama barabarani watakaobainika kuomba au kupokea rushwa kutoka kwa wananchi ili kuepuka kuwachukulia hatua kwa makosa ya usalama barabarani na pia amewaasa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa pale wanaposhawishiwa na wananchi. Hatua hii ni ya kuigwa na wadau wengine hasa ikizingatiwa kwamba MKAKATI WA KITAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI (NATIONAL ANTI CORRUPTION STRATEGY AND ACTION PLAN) inamtaka kila mdau kuhakikisha kuwa anajiwekea mikakati ya kudhibiti rushwa katika eneo lake.

Tunapenda kuwahakikishia wakazi wa mkoa wa Arusha kwamba, TAKUKURU imejipanga kuwachukulia hatua za kisheria wananchi watakaobainika kuwashawishi au kuwahonga askari wa usalama barabarani kwa lengo la kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria pale wanapokiuka sheria za usalama barabarani.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inaendelea kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa ushirikiano wanaoutoa kwa taasisi yetu kwa kutoa taarifa za wanaojihusisha na vitendo vya Rushwa na kuwataka kuendelea na moyo huo.

TAKUKURU inawahakikishia kuwa taarifa zitakazopokelewa zitafanyiwa kazi kwa haraka. Aidha kwa upande mwingine TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawaonya watu wote na watumishi wa umma wanaotafuta kujipatia manufaa kwa njia za udanganyifu. Ofisi haitasita kumkamata na kumchukulia hatua mtu yeyote.

Imetolewa na

Frida Wikesi

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha